# TAARIFA KWA UMMA

## KUSITISHWA KWA USAJILI WA WANACHAMA WA PSPTB

**Dodoma Aprili 19, 2023.**

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), inawataarifu wanachama wote ambao hawajalipa ada za uanachama kwa zaidi ya miaka miwili kuwa watasitishiwa uanachama wao ifikapo tarehe 30 Juni. 2023.

Sambamba na hili, PSPTB inatarajia kusitisha uanachama kwa wanachama wote ambao hawajahuisha taarifa zao hivyo kukwamisha utendaji wa PSPTB katika kutekeleza maelekezo mbalimbali ya Serikali.

Endapo mwanachama atakayefutiwa usajili wake ni mwajiriwa wa sekta ya umma au binafsi, hataruhusiwa kuendelea kufanyakazi za ununuzi na ugavi kwa kuwa hatatambuliwa na Bodi iliyomsajili (PSPTB), hivyo mamlaka yake ya ajira itataarifiwa kwa hatua stahiki.

Kwa wale ambao watasitishiwa uanachama wao, majina yao yatatangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii ya PSPTB.

**Imetolewa na:**

Shamim A. Mdee

**MENEJA MASOKO NA UHUSIANO - PSPTB**

**Mkandarasi Place (Ghorofa ya saba), S.L.P. 2663,Postcode 41108 Dodoma**

Simu: **+255 22 2865860** | Nukushi: **+255 22 2862138**

PSPTB TV | Bodi Ununuzi | psptbofficial | www.psptb.go.tz | info@psptb.go.tz